## 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Utangulizi

Ingawa matokeo ya jumla ya somo la Kiswahili katika mwaka wa 2019 yameimarika, utendaji wa asilimia kubwa ya wanafunzi unaelekea kuwa hafifu. Hili linadhihirika kwa matokeo ya karatasi ya tatu, ambayo yamekuwa yakishuka mwaka baada ya mwingine tangu 2016. Watahini wamekuwa wakishuhudia kushuka kwa viwango vya majibu yanayotolewa na watahiniwa. Kadhalika, kumekuwa na kushuka na kupanda kwa asilimia ya watahiniwa wanaotuzwa gredi za juu. Uchanganuzi huu unanuiwa kutathmini utendaji wa watahiniwa katika karatasi mahususi, na katika somo la Kiswahili kwa jumla. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika kipindi cha miaka minane (2012 hadi 2019).

**Jedwali 9**: ***Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili (2012 – 2019)***

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama ya Wastani | Alama Tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2012 | 1 | | 40 | 10.43 | 3.63 |
| | 2 | | 80 | 29.06 | 10.77 |
| | 3 | | 80 | 32.14 | 15.15 |
| | Jumla | 433,886 | 200 | 71.62 | 25.71 |
| 2013 | 1 | | 40 | 18.46 | 5.44 |
| | 2 | | 80 | 29.92 | 12.68 |
| | 3 | | 80 | 34.82 | 14.92 |
| | Jumla | 445,555 | 200 | 83.19 | 29.77 |
| 2014 | 1 | | 40 | 20.17 | 5.26 |
| | 2 | | 80 | 32.27 | 12.60 |
| | 3 | | 80 | 42.93 | 15.81 |
| | Jumla | 482,122 | 200 | 95.36 | 29.88 |
| 2015 | 1 | | 40 | 20.86 | 5.19 |
| | 2 | | 80 | 36.12 | 13.50 |
| | 3 | | 80 | 38.80 | 15.38 |
| | Jumla | 521,159 | 200 | 95.76 | 31.02 |
| 2016 | 1 | | 40 | 18.23 | 5.53 |
| | 2 | | 80 | 34.11 | 13.83 |
| | 3 | | 80 | 25.67 | 12.87 |
| | Jumla | 571,176 | 200 | 77.97 | 29.07 |
| 2017 | 1 | | 40 | 18.84 | 5.23 |
| | 2 | | 80 | 25.45 | 11.79 |
| | 3 | | 80 | 25.15 | 13.42 |
| | Jumla | 610,392 | 200 | 69.43 | 27.49 |
| 2018 | 1 | | 40 | 16.98 | 4.82 |
| | 2 | | 80 | 27.22 | 10.88 |
| | 3 | | 80 | 22.20 | 11.95 |
| | Jumla | 659,465 | 200 | 66.40 | 24.76 |
| 2019 | 1 | | 40 | 19.88 | 5.43 |
| | 2 | | 80 | 36.50 | 12.64 |
| | 3 | | 80 | 21.08 | 12.64 |
| | Jumla | 694,982 | 200 | 77.46 | 28.03 |

Kutokana na jedwali hili, pamoja na takwimu na ripoti nyingine za uchanganuzi wa karatasi za mitihani ya Kiswahili ya mwaka huu, imedhihirika kwamba kwa jumla:

i) Utendaji wa wanafunzi katika utungaji umeimarika. Haya yanadhihirishwa na kupanda kwa alama wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) kutoka **16.98** mwaka 2018 hadi **19.88** mwaka huu . Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **37/40.** Ni mwanafunzi **mmoja** tu ambaye alipata alama hii. Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi **(47,790)** ni **23/40.** Hali kadhalika, idadi ya wanafunzi ambao walipata asilimia sabini **(70%)** yaani **28/40** ilipanda kutoka **4,221** mwaka **2018** hadi **18,718 (2.69%)** mwaka huu .

ii) Hata hivyo, changanuzi umedhihirisha kwamba bado kuna idadi ya wanafunzi **(689)** waliopata alama moja**( 1).** Hakika wanafunzi **6,834 (0.98%) walipata** baina ya alama 1 **na 5.** Pia karatasi ya kwanza bado haijawatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Hili linadhihirishwa na alama tenganisho **(5.43. )** ambayo iko chini sana ikilinganishwa na alama ya tenganisho ya kikaida **( 15.00).** Hali hii inaweza kusababishwa na watahini kuongozwa na kutawaliwa na mtazamo nafsi wakati wa kuzitathmini insha za watahiniwa na kuishia kuwaweka katika viwango sawa au vinavyokaribiana.

iii) Alama ya wastani ya karatasi ya pili (102/2) imepanda kwa pointi **9.28** kutoka **27.22** mwaka 2018 hadi **36.50** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **76/80.** Ni mwanafunzi **mmoja** tu ambaye alipata alama hii. Wanafunzi **180** walipata baina ya alama **70/80** na **76/80.** Aidha alama iliyotuzwa wanafunzi wengi **( 20, 054)** ni **38/80.** Hali kadhalika, idadi ya wanafunzi waliopata asilimia sabini **(70%)** yaani **56/80** katika karatasi hii ilipanda kutoka **1,007** hadi **8,140 (1.17%).** Aidha, imebainika kwamba karatasi hii iliweza kuwatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Alama tenganisho ilikuwa **12.64** kinyume na **10.88,** ya mwaka 2018.

iv) Hata hivyo , bado kuna asilimia ya wanafunzi ambao walipata alama za chini. Kwa mfano, wanafunzi **3,616** walipata baina ya alama **1** na alama **5** . Hali kadhalika, ruwaza za matokeo zaonyesha kuwa matokeo ya karatasi hii yamekuwa yakiyumba tangu mwaka wa 2009. Alama ya wastani ilishuka kwa takriban alama **kumi (10)** mwaka 2010, ikapanda kwa takriban kiwango hichohicho mwaka 2011, na baadaye kushuka kwa alama **kumi na nne nukta thelathini** (**14.30** ) mwaka 2012. Mwaka 2013 ilipanda kwa kiasi kidogo mno, mwaka 2014 kwa **2.35,** na mwaka 2015 kwa takriban alama **4**. Mwaka 2016 alama ilishuka kwa takriban alama mbili. Mwaka 2017 alama hii ilishuka kwa zaidi ya alama 8. Mwaka 2018 alama wastani ilipanda kwa takriban alama **2** na mwaka huu imepanda kwa alama **9.28.**

v) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2019 yameshuka kwa takriban alama **1.12** kutoka alama wastani **22.20** mwaka 2018 hadi **21.08** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliytuzwa ni **72/80.** Ni mwanafunzi **mmoja** tu **aliyepata** alama hii.. Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi **(25,895)** ni alama **01/80 (3.73%).** Hii inamaanisha kwamba wanafunzi hawa walipata sufuri katika kila swali. Aidha wanafunzi **79,732 (11.47%)** walipata baina ya alama **1** na **5** jambo linalodokeza kwamba wanafunzi hawa hawakusoma vitabu vya fasihi. Hali kadhalika, ni wanafunzi **646** tu ambao walipata asilimia sabini **( 70%)** yaani **56/80** katika karatasi hii. Hii ni asilimia ndogo mno **( 0.09%)** ya watahiniwa **694,982** ambao walifanya mtihani huu.

vi) Alama wastani ya somo la Kiswahili kwa jumla imepanda kwa alama **11.06** kutoka **66.40** mwaka 2018 hadi **77.46** ya mwaka huu.

vii) Kadhalika asilimia ya watahiniwa wanaopata gredi A na A- ilipanda, japo haijafikia kiwango cha kuridhisha.

viii) Alama wastani ya somo hili bado haijafikia kiwango cha kuridhisha **(100/200).**

**Uchanganuzi wa karatasi mahususi**

### 3.2.2 Insha (102/1)

***Jedwali 10: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka 2012– 2019***

| Mwaka | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 10.43 | 18.46 | 20.17 | 20.86 | 18.23 | 18.84 | 16.98 | 19.88 |
| Alama ya Tenganisho | 3.63 | 5.44 | 5.26 | 5.19 | 5.53 | 5.23 | 4.82 | 5.43 |

Jedwali hili laonyesha kwamba kwa kipindi cha miaka minne (2016 - 2019), utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii umekuwa ukiyumba. Tathmini ya kazi halisi za watahiniwa imebainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa haimudu kujieleza kwa lugha iliyokomaa. Ni wazi kwamba idadi kubwa ya watahiniwa haikuweza kukuza mada inavyostahili. Aidha, asilimia kubwa ya watahiniwa ililipata chini ya nusu ya alama zilizotengewa karatasi hii yaani **19/40**. Tathmini ya kazi za watahiniwa pia imeonyesha kwamba watahiniwa wengi hawamudu tungo za kiuamilifu. Wengi wanazingatia muundo wa tungo hizi bila kushughulikia maudhui ya swali kikamilifu. Kwa mfano ingawa swali la kwanza liliwahitaji watahiniwa kuonyesha umuhimu wa vyuo vya kiufundi, wengi walipotoka, walijadili mikakati ambayo serikali na washikadau wanapaswa kuzingatia ili kuviboresha vyuo hivi. Kadhalika wanafunzi hawamudu maswali yanayoshughulikia masuala mtambuko. Asilimia kubwa ya watahiniwa haikuweza kuonyesha umuhimu wao katika kujihakikishia usalama. Hii ni ishara kwamba wanafunzi wengi, ama wamekosa ubunifu, au hawana mazoea ya kusoma kwa kina na kwa mapana. Kadhalika imebainika kwamba swali linalohusu methali halipendelewi na wanafunzi wengi. Idadi ya watahiniwa walioteua swali lililohusiana na methali ilikuwa chini. Hili linadokeza kwamba ule mtazamo wa kijadi kuwa insha zinazohusu methali huwa ngumu bado umekita mizizi.

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.

**1. Lazima**

> Wewe ni Mkuu wa Elimu katika kaunti ndogo ya Tuangaze. Andika hotiba utakayowatolea Maafisa wa Elimu na Walimu Wakuu kuhusu umuhimu wa kustawisha vyuo vinanyotoa mafunzo ya kiufundi katika eneo lao.

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuandika hotuba kuhusu umuhimu wa vyuo vinavyotoa mafunzo ya kiufundi

Hata hivyo, tungo za watahiniwa zilidhihirisha kwamba wengi wamekosa ubunifu. Wengi hawakuweza kujadili hoja zilizotarajiwa; wakashindwa kukuza mada kikamilifu. Ni muhimu kukumbuka kuwa watahiniwa walikosa ubunifu hata katika maswali yale mengine.

Imebainika kwamba wanafunzi wengi hawasomi kwa mapana, hivyo hawadiriki kushughulikia masuala mtambuko ipasavyo katika tungo zao.

#### 3.2.2.1 Ushauri kwa walimu

Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote bila ubaguzi, kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, Kenya (KICD).

KCSEREVISION.COM

**3.2.2.2 Mapendekezo**

i) Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.

ii) Walimu watumie silabasi ya K.I.C.D ili kuelekeza ufundishaji wao. Mwongozo unaotolewa na KNEC kuhusu mada na stadi zinazotahiniwa, pamoja na vitabu vya Fasihi vinavyotahiniwa, utumiwe kujalizana na silabasi ya KICD.

iii) Wanafunzi wahimizwe kusoma kwa mapana, na kwa kina (magazeti, majarida, kazi za kifasihi, na vitabu katika nyanja anuwai) ili kujifahamisha kuhusu matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao, kitaifa na pia kimataifa. Hili litapalilia ubunifu wao na kuwawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala mtambuko iwapo yatatahiniwa. Haitoshi kujifunga katika masuala yaliyo vitabuni pekee.

iv) Wanafunzi waongozwe na kuelekezwa kuhusu mikakati ifaayo ya kufasiri maswali. kwa uangalifu mkubwa huku wakizingatia maneno muhimu.

**3.2.3 Lugha (102/2)**

**Jedwali 11**: ***Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka 2012 hadi 2019***

| Mwaka | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 29.06 | 29.92 | 32.27 | 36.12 | 34.11 | 25.45 | 27.22 | 36.50 |
| Alama ya Tenganisho | 10.77 | 12.68 | 12.60 | 13.50 | 13.83 | 13.42 | 10.88 | 12.64 |

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yameimarika kutoka **27.22** mwaka 2018 hadi **36.50** mwaka huu. Swali la kwanza liliwatatiza baadhi ya watahiniwa; hawakumudu maswali yaliyowahitaji kutumia ujuzi wao kupata majibu. Haya ni maswali yanayolenga kukuza stadi za kiwango cha juu cha utambuzi kama vile uchanganuzi, usanisi na tathmini. Tutachanganua swali la tatu.

3. **MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

(a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (alama 2)

(i) irabu, konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu

(ii) konsonanti, konsonanti, irabu, irabu

(b) Ainisha mofimu katika maneno yafuaatayo: (alama 2)

(i) asemavyo

(ii) mwangwi

(c) Onyesha aina za nomino katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Shule nzima ilifurahia ukarimu wa Shirika la Tugawane.

(d) Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)

Seremala aliulainisha ubao huo ili kutengeneza kasha amuuzie mlinzi huyo.

(e) Tunga sentensi ukitumia vivumishi vinavyotoa maana zifuatazo:

(i) Nafasi katika orodha (alama 1)

(ii) Kutobagua (alama 1)

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa. (alama 1)

Mtu huyo alifuata njia iliyomwelekeza mjini.

(g) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo bila kupoteza maana.

(i) Mhandisi alikarabati mtambo.
Mtambo ulikuwa kiwandani.
(Unganisha kuwa sentensi moja bila kutumia kiunganishi.) (alama1)

(ii) Kembo alishona fulana hiyo vizuri sana. (Tumia kielezi cha kiasi badala ya vile vilivyopigiwa mstari.) (alama 1)

(h) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (alama 2)

Mkurugenzi alisema kwamba wangetoa nyongeza ya mshahara mwaka ambao ungefuata.

(i) Geuza sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu. (alama 1)

Ni wazi kwamba gharama ya maisha itapanda bei ya mafuta ikipanda.

(j) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi. (alama 1)
Badi huwa hapitii hapa, huenda usimpate.

(k) Zuri ni kwa baya, aminifu ni kwa ................ na vivu ni kwa ............... (alama 2)

(l) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)

(i) sukari ..........................................................................................................

(ii) teo ..............................................................................................................

(m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari. (alama 2)

Mvua imepusa na watu wameanza kuondoka.

(n) Vyakula viliandaliwa. Vyakula vilikuwa na viinilishe muhimu.
(Unganisha kuunda sentensi changamano.) (alama 2)

(o) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Zumari alimtunzia Keto watoto hao kwa upendo.

(p) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi 'ku'. (alama 2)

(q) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Usalama ukiimarishwa watalii wengi watakuwa wanazuru humu.

(r) Unaporidhika na jambo unasema hewala, unaposhangilia timu yako kwa kupata ushindi
unasema ........................ na unapotaka usikivu unasema ..................... (alama 2)

(s) Jepesi ni kwa rahisi, ukuta ni kwa ............... na njia ni kwa .................. (alama 2)

(t) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya dua na tua. (alama 2)

(u) Mzee Pumu ni mraibu wa vileo. Baada ya muda watoto wake wawili wanakuwa watumizi sugu wa vileo. Andika methali inayoweza kutumiwa kuelezea hali hii. (alama 1)

(v) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha uteuzi. (alama 1)

Maswali katika sehemu hii yalilenga mada mbalimbali za kisarufi kama zilivyopendekezwa kwenye silabasi.Maswali yalimhitaji mtahiniwa kutumia ujuzi wake wa dhana za kisarufi kujibu maswali aliyopewa. Imebainika kwamba utendaji wa wanafunzi katika dhana za kimsingi za lugha kama vile kuandika katika umoja, njeo, aina za maneno, na mnyambuliko wa vitenzi unaendelea kuwa hafifu. Kadhalika, watahiniwa wengi walipoteza alama katika maswali maalum, hata ya ufahamu na ufupisho, kutokana na makosa ya sarufi na hijai. Wengine hawakumudu kuandika ufupisho ipasavyo; walinakili yale yaliyokuwa katika kifungu, na kuishia kupoteza alama kwa kuzidisha idadi ya maneno. Isitoshe, wanafunzi wengi, japo walielewa sajili ya kidini hawakumudu kulishughulikia swali hili (swali la 4) kwa kina kwa kupungukiwa na hoja.

### 3.2.3.1 Mapendekezo

i) Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi katika vipengele vyote vya kisarufi.

ii) Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama vile matumizi/ utekelezaji na usanisi. Wasitarajie kila mara kupata maswali ya kuchopoa majibu moja kwa moja kutoka kwenye vifungu au kukariri kutoka kumbukumbu zao.

iii) Wanafunzi wapewe mazoezi ya ufahamu na muhtasari mara kwa mara huku wakihimizwa kuzingatia mtiririko ufaao ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.

iv) Walimu wasisitize vipengele vya kimsingi vya sarufi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.

v) Mwelekeo mseto katika ufunzaji uzingatiwe zaidi. Mathalan mwalimu anaweza kutumia Fasihi kufunzia mada tata za sarufi, kama vile aina za sentensi. Hili litachangia katika kulihuisha somo la sarufi na kuwafanya wanafunzi kulichangamkia.

vi) Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.

vi) Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wayo bila kubagua.

KCSEREVISION.COM

### 3.2.4 FASIHI (102/3)

**Jedwali 12**: *Matokeo ya Karatasi ya tatu (102/3) ya miaka 2012 hadi 2018*

| Mwaka | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 32.14 | 34.82 | 42.93 | 38.80 | 25.67 | 25.15 | 22.20 | 21.08 |
| Alama ya Tenganisho | 15.15 | 14.92 | 15.81 | 15.38 | 12.87 | 13.42 | 11.95 | 12.64 |

Matokeo haya yanaonyesha kuwa utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii unaendelea kudorora. Idadi kubwa (25,895) ya wanafunzi ilipata alama **1/80**. Hali kadhalika, karatasi za watahiniwa zimebainisha kwamba changamoto kuu inayoukumba utendaji wa wanafunzi katika fasihi ni kutosoma vitabu viteule. Ithibati ya haya ni kuchanganya kwa wahusika; mtahiniwa akajadili sifa za mhusika mwingine badala za yule aliyelengwa na swali. Kadhalika karatasi zilibainisha kutomudu maswali ya kimuktadha, pamoja na yale ambayo yanamhitaji mwanafunzi kujadili umuhimu wa vipengele vya kiploti kama vile mandhari na mbinu rejeshi katika kuvijenga vipengele vingine vya kazi husika kama vile wahusika na maudhui. Yaelekea kwamba ujifunzaji wa fasihi simulizi ni hafifu. Watahiniwa wengi hawakulimuidu swali la fasihi simulizi, hasa lile lilitowahitaji kuainisha wimbo na kujadili mbinu mwafaka za kuzifanyia nyimbo za aina hii utafiti.

Hali kadhalika, tathmini ya karatasi halisi za watahiniwa ilibainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa, hata wale wanaopata alama za juu zaidi katika karatasi hii, haimudu kuwasilisha hoja kwa njia komavu. Kazi za watahiniwa zimepwezwa na makosa mengi ya kisarufi, kimuundo na hijai. Kadhalika, pameibuka mtindo wa kuwasilisha hoja kwa ufupi mno, bila kuzitolea mifano kutoka matini husika ya kifasihi. Hili linawafanya watahiniwa wengi kupoteza alama. Vile vile maswali ya ushairi yanaepukwa na watahiniwa wengi. Hata wale wanaodiriki kuyafanya, wanaambulia alama za chini. Imebainika kwamba baadhi ya masuala ya kimsingi ya ushairi hayafunzwi, hivyo yanapotokea katika mtihani watahiniwa wengi hupoteza alama. Wanafunzi wanaonekana kukariri dhana za kishairi bila kuzielewa. Hawamudu kutumia ujuzi wa dhana hizi kujibia maswali.

Tutachanganua swali la kwanza kwani ndilo lililokuwa la lazima.

**A. Matei:** *Chozi la Heri*

**1. Lazima**

(a) "Sasa haya ameyapa kisogo ... kufunguliwa kwa kituo hiki ni kama mana iliyomdondokea kinywani kutoka mbinguni."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Bainisha tamathali **mbili** za usemi ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

(iii) Fafanua umuhimu wa mhusika anayerejelewa katika dondoo hili katika kuijenga riwaya hii. (alama 6)

(b) Jadili mikakati mwafaka ambayo vijana wanatumia kukabiliana na hali yao ya maisha kwa kuwarejelea wahusika wafuatao:

(i) Chandachema (alama 4)

(ii) Dick (alama 4)

Hili lilikuwa swali la kimuktadha ambalo lilimhitaji mwanafunzi kuwa ameisoma riwaya na kuelewa ploti ili kubainisha msimulizi na mandhari katika riwaya ambamo kauli ilitolewa. Swali hili pia lihitaji mwanafunzi kuonyesha mwingiliano uliopo kati ya vipengele vya kazi ya kifasihi, hasa umuhimu wa wahusika katika kuijenga kazi ya kifasihi.

Hata hivyo uchanganuzi wa utendaji wa wanafunzi katika swali hili, na hata katika maswali mengine ulidhihirisha kwamba wanafunzi hawasomi vitabu vya fasihi kwa kina. Watahiniwa hawakuweza kuliweka dondoo katika muktadha. Pia, hawakuweza kufafanua umuhimu wa wahusika. Kadhalika, wanafunzi wengi hawazielewi istilahi za kimsingi za uchambuzi wa kazi za kifasihi. Kwa mfano, watahiniwa wengi walishindwa kuelewa maana ya **mtindo** katika swali lilowahitaji kuchanganua vipengele vya kimtindo katika dondoo walilopewa.

### 3.2.5 MAPENDEKEZO

i) Walimu wawaongoze wanafunzi kujifunza vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu huku wakizingatia vipengele vifuatavyo vya uchanganuzi wa kazi za kifasihi:
   a) Dhamira na maudhui
   b) Fani, kama vile:
      - Mandhari- Maana na umuhimu wayo
      - Ploti- vipengele kama vile mbinu rejeshi, elekezi na sadfa, na umuhimu wavyo
      - Usimulizi- nafsi na wakati katika usimulizi
      - Wahusika- Sifa na umuhimu wao katika kuzijenga kazi za kifasihi
      - Muundo- urudiaji, usambamba....
      - Mtindo, kama vile tamathali za usemi, urudiaji, n.k

ii) Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika diwani teule ya hadithi fupi.

iii) Wanafunzi wawekewe misingi bora katika Fasihi Simulizi tangu kidato cha kwanza na kuongozwa kujiimarisha katika mada zote za fasihi simulizi kulingana na upeo uliopendekezwa na, mtaala wa shule za upili.

iv) Walimu wawaelekeze wanafunzi wao kutambua na kutumia istilahi muhimu za ushairi ili kuupalilia ukakamavu wao katika kuyajibu maswali ya Ushairi.

v) Mbinu za kuchanganua Ushairi zifunzwe katika upana na kina kulingana na kiwango hiki.

vi) La muhimu zaidi wakumbushwe kwamba vipengele vya kazi ya kifasihi havitofautiani. Mathalani, taswira na toni huweza kuchanganuliwa katika Ushairi, na vilevile katika tamthilia na tungo za kinathari, kama vile riwaya.

### 3.2.6 Hitimisho

Kutokana na uchanganuzi wa hapo juu, ni dhahiri kwamba japo utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa jumla umeimarika mwaka huu, matokeo ya karatasi ya tatu bado yanaendelea kushuka. Asilimia kubwa mno ya watahiniwa imepata tuzo za chini, hali ambayo imeshusha alama ya wastani ya karatasi hii na ya somo zima. Vilevile ni dhahiri kwamba matokeo ya watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa jumla bado hayajafikia kiwango cha kuridhisha.

Inatumainiwa kwamba walimu na wanafunzi watafaidi kwa uchanganuzi uliotolewa. Kadhalika ni muhimu kuyatilia maanani mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ili kuimarisha matokeo ya somo hili. Muhimu zaidi, ipo haja ya kuandaa warsha na makongamano ili kufanikisha kujadiliwa kwa mada na stadi ambazo zinaelekea kuwatatiza zaidi walimu na wanafunzi.